

Jumatao 11 Machi 18, 2026

194.



Aidha, kwa waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda, wanatakiwa kuendesha kwa tahadhari wakiheshimu waendesha magari ya binafsi na abiria kuepuka kusababisha ajali.



Na SUPERIUS ERNEST

Wananchi wazingatie sheria kuepusha ajali za barabarani

WAPO wanaofahamu kuwa jukumu la kuzingatia sheria barabarani ni la madereva peke yao, jambo ambalo siyo sahihi.

Utii wa sheria na kanuni hizo ni muhimu kwa kila mmoja kuepuka ajali barabarani ambazo hupoteza uhai wa watu na kuharibu mali.

Ni kweli madereva wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kufuata na kuzingatia sheria na alama za barabarani na wananchi wanawajibika pia kutii sheria hizo kwa usalama wao.

Mfano madereva wanapofika katika alama za kuvuka kwa watembea kwa miguu, wanatakiwa kupunguza mwendo na kutazama kama kuna mwananchi anayetaka kuvuka.

Vilevile wananchi wanapofika katika maeneo hayo wanatakiwa kusimama na kuangalia kama kuna gari au chombo kingine cha usafiri kinapita, kisha wavuke.

Lengo la kufanya hivyo ni kuepuka ajali zisizo za ulazima barabarani, iwe kwa dereva au mtembea kwa miguu.

Katika muktadha huo, madereva

wanaoendesha vyombo mbalimbali vya moto wanatakiwa kuwa makini kwa kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, wasiwe sababu kwa madereva wengine kupata ajali.

Mfano, waendesha magari ya usafirishaji wanatakiwa kuzingatia umakini wao kwa wao hususan katika kupishana au kumpita dereva mwingine.

Pia, madereva wa mabasi ya abiria na wale wa binafsi wanatakiwa kuheshimia na kuendesha kwa umakini, hususan katika 'Ku Over take'

Aidha, kwa waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda, wanatakiwa kuendesha kwa tahadhari wakiheshimu waendesha magari ya binafsi na abiria kuepuka kusababisha ajali.

Vivyo hivyo, kwa waendesha magari kuwaheshimu waendesha pikipiki na baiskeli, kwani wote wana haki ya kutumia barabara hizo.

Maelekezo hayo, yamekuwa yakisisitizwa na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP William Mkonda, kuwa jukumu la utii wa sheria barabarani ni la kila mmoja

pasipo kujalisha ni dereva, abiria au mtembea kwa miguu.

Aidha amekuwa akisisitiza madereva wote wa magari ya abiria, pikipiki, bajaji kuwa makini na kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, kwani kwa kufanya hivyo ndiyo tutaepuka na kupunguza ajali.

Anasema dereva makini siyo yule anayeendesha kwa kasi kubwa, bali ni yule anayeendesha kwa tahadhari na kufuata sheria, taratibu, kanuni na alama za barabarani, hali inayopunguza ajali sizizo na sababu.

Ni vyema kila mmoja akazingatia msisitizo huo, kwa kuwa utasaidia kupunguza ajali za barabarani.

Pia, utaimarisha utaratibu barabarani kama magari kusimama katika vituo vyake maalumu, bajaji na pikipiki.

Ikumbukwe kuwa kuzingatia sheria barabarani siyo tu, kwamba ina matokeo ya kuepusha ajali bali, inalinda uhai wa kila mmoja na kuwaweka salama wategemezi wake.